KIJALIZO CHA SHERIA NDOGO NAMBARI 1 **Tarehe 12 Febuari, 2010**

KIJALIZO CHA SHERIA NDOGO
kwenye Gazeti Maalum la Uganda Nambari 10 Juzuu CIII iliyotolewa
tarehe 12 Febuari, 2010

Ilipigwa chapa na UPPC, Entebbe, chini ya Amrisho la Serikali

Sheria ndogo 1 *(Marekebisho ya) Sheria ya Ardhi* **2010**

(MAREKEBISHO YA) SHERIA YA ARDHI, 2010

MPANGILIO WA SEHEMU.

Sehemu

1. Marekebisho ya sehemu 31 ya sheria ya ardhi.
2. Uingizaji wa sehemu mpya ya 32A.
3. Marekebisho ya sehemu 35 ya sheria kuu.
4. Marekebisho ya sehemu 59 ya sheria kuu.
5. Marekebisho ya sehemu 92 ya sheria kuu.

Sheria ndogo 1 *(Marekebisho ya) Sheria ya Ardhi* **2010**

(MAREKEBISHO YA) SHERIA YA ARDHI, 2010

Sheria ndogo ya kuidhinisha kurekebisha Sheria ya Adhi ili kuhakikisha na kuimarisha ukaaji salama wa wakaaji wa kweli na wa kisheria katika ardhi iliyosajiliwa kwa mujibu wa kifungu 237 cha Katiba, na mambo mengineyo yanayohusika.

TAREHE YA KUIDHINISHWA: 6 Januari, 2010.

Tarehe ya kuanzisha: 12 Februari, 2010.

ILITUNGWA na Bunge kwamba:

Disclaimer
The Original of this translation is the English text of the Law which is the only authentic version for purposes of enforcement of the Law.

1. **Marekebisho ya sehemu 31 ya Sheria ya Ardhi.**
Sehemu 31 ya Sheria ya Ardhi, ambayo katika Sheria hii inarejelewa kama Sheria kuu, imefanyiwa mageuzo–

a) kwa kuingiza moja kwa moja baada ya sehemu ndogo (3c), yafuatayo – "(3c) Endapo bodi haijaamua ushuru wa ardhi wa kwanza wa kila mwaka unaolipwa na mpangishaji mkaaji mnamo miezi sita baada ya kuanzishwa kwa (Marekebisho ya) Sheria ya Ardhi ya 2010, ushuru huo unaweza kuamuliwa na Waziri.

(3e) Ushuru wa ardhi unaolipwa chini ya sehemu hii utalipwa mnamo mwaka mmoja baada ya Waziri kuidhinisha ushuru wa kulipwa chini ya sehemu ndogo (3) au ushuru alioamuwa ulipwe chini ya sehemu ndogo (3d).";

(b) katika sehemu ndogo (6), kwa kubadilishana maneno "miaka miwili" na badala yake kuweka "mwaka mmoja".

2. **Uingizaji wa sehemu mpya ya 32A**

Sheria kuu imegeuzwa kwa kuingiza yafuatayo moja kwa moja baada ya sehemu 32, yafuatayo–

"32A. Wakaaji wa kweli au wanaokubalika kisheria wataondolewa tu kutoka ardhi wakishindwa kulipa ushuru wa ardhi.

(1) Mkaaji wa kweli au aliyeidhinishwa kisheria hataondolewa kutoka ardhi iliyosajiliwa ila tu kukiwa na amri ya kumwondoa iliyotolewa na mahakama na kwa sababu tu ya kushindwa kulipa ushuru wa ardhi wa kila mwaka uliowekwa.

(2) Mahakama, kabla ya kuidhinisha amri ya kuondoa mtu kutoka ardhi chini ya sehemu hii, itazingatia mambo yaliyobainishwa katika sehemu 32(1)

(3) Wakati wa kutoa amri ya kuondoa mtu kutoka ardhi, mahakama itaandika katika amri hiyo, tarehe, ambayo haitakuwa chini ya miezi sita baada ya amri hiyo, ambayo mtu anayeondolewa kutoka ardhi ataacha ardhi hiyo na mahakama inaweza kutoa amri yoyote kuhusu gharama, mali iliyoharibiwa, fidia au jambo lolote jingine ambalo mahakama itafikiria kuwa ni mwafaka.

(4) Kwa madhumuni ya sehemu hii, neno "Mahakama" litakuwa na maana ya mahakama inayoongozwa na Hakimu wa daraja la kwanza au Hakimu Mkuu kutegemea yeyote atakayehusika, na rejeo kwenye

Disclaimer
The Original of this translation is the English text of the Law which is the only authentic version for purposes of enforcement of the Law.

Koti ya Ardhi katika Sheria kuu na marekebisho yake yatafasiliwa katika msingi huo.

3. Marekebisho ya sehemu 35 ya Sheria kuu.

Sehemu 35 ya sheria kuu imefanyiwa marekebisho-

(a) kwa kuingiza papo hapo yafuatayo baada ya sehemu ndogo (1)-

"(1a) Licha ya kuzingatia sehemu ndogo (7), mpangisha anayekaa kwenye ardhi anayeamua kupangisha ardhi kwa mkaaji mwingine bila ya kutoa nafasi hiyo kwanza kwa mwenye ardhi mwenewe huwa amefanya kosa na anakupewa adhabu ya kulipa pesa zisizozidi pointi tisini na sita za thamani ya hela (shilingi milioni moja, laki tisa na ishirini elfu) au kufungwa jelani kifungo kisichozidi miaka minne au kupewa adhabu zote mbili; na shughuli hizo za kupangisha ardhi zitafutwa, kisha mkaaji huyu atatolewa haki ya ukaaji kwenye ardhi hiyo na ardhi hiyo itarudishiwa mwenye ardhi aliyesajiliwa.

(b) kwa kuingiza papo hapo yafuatayo baada ya sehemu ndogo (7)-

"(8) Licha ya kuzingatia sehemu hii, kubadilisha umilikaji wa ardhi iliyosajiliwa uliofanywa na mmilikaji baada ya kuuza, kutoa kama zawadi au kurithisha ardhi yake hakutaathiri mkaaji wa kweli au wa kisheria kwa njia yoyote ile na mmilikaji mpya atalazimika kuheshimu haki na maslahi ya wakaaji kwenye ardhi hiyo."

4. Marekebisho ya sehemu 59 ya Sheria kuu.

Sehemu 59 ya sheria kuu imefanyiwa marekebisho kwa kuingiza papo hapo yafuatayo baada ya sehemu ndogo 59(1)-

"(1A) endapo bodi imekubali, imeidhinisha au kukamilisha shughuli za uuzaji au utoaji na ugawaji ardhi unaopingana na sehemu ndogo (1)(a), shughuli hizo zitakuwa haramu na zitafutwa."

5. Marekebisho ya sehemu 92 ya Sheria kuu.

Sehemu ya 92 ya sheria kuu imerekebishwa kwa-

(a) sehemu ndogo (1) ya sehemu 92 imerekebishwa kwa kuanzisha sheria ndogo mpya papo hapo baada ya sehemu ndogo (1) aya (d) kwamba-

"(e) kujaribu kuondoa, kutekeleza kuondoa au kushiriki katika kuondoa mkaaji wa kweli au aliyeidhinishwa kisheria kutoka ardhi iliyosajiliwa bila ya kuwa na amri kutoka mahakama;"

Disclaimer

The Original of this translation is the English text of the Law which is the only authentic version for purposes of enforcement of the Law.

(b) kubadilishana sehemu ndogo (4) na kuweka yafuatayo-

"(4) Mtu aliyehukumiwa kosa linalobainishwa katika sehemu ndogo (1) (c) anapewa adhabu ya kulipa hela zisizozidi pointi tisini na sita za thamani ya hela (shilingi milioni moja, laki tisa na ishirini elfu) au kufungwa jelani kifungo kisichozidi miaka minne au adhabu zote mbili."

(c) sehemu 92 inarekebishwa kwa kuingiza moja kwa moja yafuatayo baada ya sehemu ndogo (5)-

"mtu aliyehukumiwa kosa linalobainishwa katika sehemu ndogo (1) (e) anapewa adhabu ya kifungo cha jelani kisichozidi miaka saba baada ya kuhukumiwa."

(d) (5B) endapo mtu amehukumiwa chini ya sehemu ndogo (5A), mahakama inaweza-

i) kuamrisha kwamba mtu huyu alipe fidia au mali zilizoharibika kwa mtu aliyeondolewa kutoka ardhi; au

ii) kutoa amri ya kurudishia mtu ardhi aliyoondolewa.

Disclaimer

The Original of this translation is the English text of the Law which is the only authentic version for purposes of enforcement of the Law.